

Jina la Mwanafunzi _____

Namba ya Upimaji _____

Mkoa _____

Wilaya _____

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

01

KISWAHILI

Muda: Saa 1:30

Mwaka: 2024

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E zenyé jumla ya maswali **matano (5)**.
2. Jibu maswali **yote**.
3. Andika majibu yote kwenye nafasi zilizoachwa wazi katika kila swali.
4. Andika majibu yote kwa kutumia kalamu ya wino wa **bluu** au **mweusi**.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vingine visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha upimaji.
6. Andika **Jina lako, Namba ya Upimaji, Mkoa na Wilaya** sehemu ya juu kulia katika kila ukurasa.

KWA MATUMIZI YA MPIMAJI TU		
NAMBA YA SWALI	ALAMA	SAINI YA MPIMAJI
1		
2		
3		
4		
5		
JUMLA		
SAINI YA MHAKIKI		



Ukurasa wa 1 kati ya 6

2024

Jina la Mwanafunzi _____

Namba ya Upimaji _____

Mkoa _____

Wilaya _____

SEHEMU A (Alama 10)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Sikiliza kwa makini sentensi zifuatazo kisha uziandike kwa usahihi katika nafasi zilizoachwa wazi.

- (i) _____
- (ii) _____
- (iii) _____
- (iv) _____
- (v) _____

SEHEMU B (Alama 10)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

2. Andika neno jipya linaloundwa kwa kudondosha silabi moja katika kila neno ulilopewa.

- (i) Mkasi _____
- (ii) Wazima _____
- (iii) Elewa _____
- (iv) Mpeni _____
- (v) Hatibu _____

Ukurasa wa 2 kati ya 6

sfna2024

Jina la Mwanafunzi _____

Namba ya Upimaji _____

Mkoa _____

Wilaya _____

SEHEMU C (Alama 10)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

3. Andika maana ya nahau katika (i) – (v) kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku na kuliandika katika nafasi iliyoachwa wazi.

tamani kitu, ipo siku utakamatwa, kuishi miaka mingi, ona aibu, mwisho wa safari, fukuzwa kazi, kuiba kitu.

- (i) Tia nanga_____
- (ii) Mezea mate_____
- (iii) Mwaga unga_____
- (iv) Kula chumvi nyingi_____
- (v) Ona haya_____

Ukurasa wa 3 kati ya 6

sfna2024

Jina la Mwanafunzi _____

Namba ya Upimaji _____

Mkoa _____

Wilaya _____

SEHEMU D (Alama 10)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

4. Kamilisha barua ya kirafiki ifuatayo kwa kuchagua jibu sahihi kutoka kwenye kisanduku kisha kuandika katika nafasi zilizoachwa wazi.

Mimi mdogo wako, Madhumuni ya barua, Shule ya Msingi
Ushindi, Ni matumaini yangu, Shikamoo.

(i) _____,

S. L. P 773,
Mwanza.

05/05/2024.

Mpendwa Kaka, (ii) _____.

(iii) _____ kwamba wote hapo nyumbani hamjambo. Mimi sijambo na ninaendelea vizuri na masomo.

(iv) _____ hii ni kukujulisha kwamba, likizo ya mwezi wa sita nitabaki shulenii ili kuijandaa na Mitihani ya Taifa. Binafsi nimedhamiria kufaulu vizuri kwa kupata gredi 'A' katika masomo yote.

Ninakutakia kila la kheri katika shughuli zako za kila siku.

(v) _____

Akilimali.

Ukurasa wa 4 kati ya 6

2024

Jina la Mwanafunzi _____

Namba ya Upimaji _____

Mkoa _____

Wilaya _____

SEHEMU E (Alama 10)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

5. Soma kwa makini habari ifuatayo kisha jibu maswali yanayofuata kwa **kuandika jibu lililo sahihi** katika nafasi iliyoachwa wazi.

Kalulu ni kijana anayeishi mtaa wa Kaloleni. Vijana wenzake mtaani walikuwa hawampendi kwa sababu ya tabia zake mbaya za kutowaheshimu wazazi wake, kuvuta bangi na wizi. Tabia mbaya ya Kalulu haikuishia mtaani kwake tu lakini hata shuleni aliendelea na tabia hizo. Walimu wake walijitahidi **kumrudi** lakini hakutaka kujirekebisha mwishowe alifukuzwa shule.

Siku moja usiku alitoroka nyumbani na kwenda kwa rafiki yake aitwaye Mashaka. Yeye pamoja na rafiki yake walikaa kichochoroni wakiwa wanavuta bangi. Polisi waliokuwa katika doria walipita katika kichochoro walichokuwa wamekaa na kuwakamata. Walipelekwa katika kituo cha polisi na hatimaye mahakamani. Hakimu alitoa hukumu na wote walifungwa katika jela ya watoto kwa miezi sita kwa kosa la kuvuta bangi na uzururaji. Baada ya kumaliza kifungo, Kalulu alibadili tabia na kuwa kijana mtiifu sana. Wazazi wake na jamii kwa ujumla walimpenda na kumwamini.

Maswali:

- (a) Kalulu ni kijana anayeishi wapi?

Ukurasa wa 5 kati ya 6

smna 2024

Jina la Mwanafunzi _____

Namba ya Upimaji _____

Mkoa _____

Wilaya _____

- (b) Neno **kumrudi** kama lilivyotumika katika habari uliyosoma lina maana gani?

- (c) Kwa nini Kalulu na Mashaka walifungwa?

- (d) Taja sababu mbili zilizofanya Kalulu kutopendwa na vijana wenzake?

(i) _____

(ii) _____

- (e) Habari uliyosoma inatoa funzo gani?
